

Hadisi ya Muheshimiwa Muke wa Kwanza Denise Nyakeru Tshisekedi



Amezaliwa tarehe 9 Machi 1967 mjini Bukavu, katika Kivu ya Kusini. Denise NYAKERU TSHISEKEDI anaolewa toka miaka makumi mbili na tatu na Raïs wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Félix-Antoine Tshisekedi Tshilombo. Ni mama mwenyi heri ya watoto watano, mwanaume mmoja na wabinti wane.

Yatima wa baba na mama, miezi kenda kisha kuzaliwa, alipokelewa pamoja na kaka na dada zake mjini Kinshasa na mjomba wake, padri mkumbwa wa Vikosi vya Jeshi ya Zaïre, Padri Sylvestre Ngami Mudahwa mwenyi alikuwa baba mlishi kwao na aliwaelimisha.

Mnamo 1985, mjomba mtenda mema akafa katika msiba ya gari. Sehemu hii ya maisha yake, pahali pa ku muvundja, ikamupa nguvu zaidi na kitumaini kubwa katika maisha. Amepata Cheti cha Serkali na ameendelea masomo yake mijini Ubelegi kwenyi alianza kazi kama mtunzaji.

Kazi yenyi alitimiza katika mapendo ya wengine, heshima, na roho ya usaidizi, tabia mema ambazo yalimjenga, yanamutambulisha na yatasimamia uchaguzi ya ahadi zake za baadaye.

Toka mumewe kufika ku Uhamuzi mkuu ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, yule anaitwaye toka hapo "Muheshimiwa Muke wa wanza", anajitolea katika kuheshimisha wanawake na wasichana wa Congo, kwa njia ya shirika "Fondation Denise Nyakeru Tshisekedi (FDNT)". FDNT, iliyoundwa mnamo Mai 2019, inashurlikia na mambo makubwa mane (4) kwa ajili ya kutimiza msimamo inayotajika huko juu. Ya kwanza, ni

afya ya wanawake, msinji ya siasa yote inayofaa. Ya pili, elimu ya wasichana, zaidi wasiyoshurlikwa na wenyi magumu. Ya tatu, kipinga hali zote za mashambulizi zinazo haribisha picha ya mwanamke na ya msichana, juu yake mwenyewe na juu ya wanaokaa naye, na wanayo niya ya kumuona bure. Na ya mwisho, uweseshaji wa kifeza kwa wanawake na wasichana yenyi kuwa kiungo ya mwisho ya mnyororo, sababu ni mwanamke tu mwenyi afya bora, mwenyi elimu bora na mwenyi kuwa mbali na hali yote ya ushambulizi, ndio anaweza kuunga mkono kwa maeldeleo ya taifa yake.

Alieteuliwa kama Balozi wema wa Mfuko ya Ulimwengu juu ya Watu (UNFPA) mnamo Mayi 2019, juu ya kipinga unyanyasaji inaoategemeya gender na uweseshaji ya wanawake, ali pewa vile vile kuwa "Bingwa wa Ulimwengu wa Kuzuia ukatili wa kijinsia zinazohusiana na vita" na Offisi ya mjumbe wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayohusika na mambo haya, mnamo Disemba 2019. Cheo hii, siyo zawadi, ila ujumbe : ya kubeba sauti ya waliyeumia na shida hii kunako maofisi za nchini, za mataifa jirani na ya Umoja ya Mataifa.